4.2 KISWAHILI (102)

4.2.1 Kiswahili Paper (102/1)

1. Lazima

   Wewe ni Mkuu wa Elimu katika kaunti ndogo ya Tuangaze. Andika hotuba utakayowatolea Maafisa wa Elimu na Walimu Wakuu kuhusu umuhimu wa kustawisha vyuo vinavyotoa mafunzo ya kiufundi katika eneo lao.

2. "Usalama wa mwanafunzi unamtegemea yeye." Jadili.

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

4. Andika kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:

   Nilimtazama kwa muda. Moyo wangu ulinituma kumuuliza kilichomfanya kuishi katika mazingira ya kudhalilisha kama hayo.

Downloaded From: https://aikaschool.org

4.2.2 Kiswahili Paper (102/2)

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kijiji chetu kilikuwa kimeanza kuingiwa na wasiwasi. Katika kipindi cha miaka michache iliyopita tulikuwa tumewapoteza watu kadha na hakuna aliyeelewa kiini hasa cha majanga haya. Wazee walisikika wakisemezana kwa sauti za chini. Hatukujua hasa walichosema lakini ilikuwa bayana kuwa kijiji chetu kilikuwa juu ya mchongoma.

Kijijini kwetu kuna mambo yatokeayo yakaonekana miujiza.Tunabaki kutapatapa kuelezea chanzo chake na wesemavyo, akili ni nywele kila mtu ana zake. Ila zipo **nywele za koto na za singa**. Lakini kuna watu wenye kuandamwa na tata, mti wowote uliokuwa karibu ulishikiliwa kwa tumaini la kuleta nafuu. Ndiyo, nafuu. Na ndivyo ilivyotokea kiasi cha kila mtu kuwa bingwa wa kufasiri asili ya janga na suluhu yake. Hali hii iliendelea mpaka walipofika wataalamu kijijini kwetu na kufanya utafiti wa kisayansi uliotufumbulia asili ya dhiki zetu.

Siku hiyo ya kutolewa matokeo ya utafiti, kijiji kizima kilijumuika kwenye uwanja wa shule mapema. Hakuna aliyeonyesha uso wa furaha. Ilikuwa kama tuliokuwa mahakamani tunasubiri hukumu ya kesi ya jinai dhidi yetu. Siyakumbuki yote aliyosema yule mtaalamu lakini yapo yaliyotugusa sote.

"Najua mna hamu ya kujua tatizo liko wapi. Kabla ya kulieleza tatizo lenyewe ningependa kusema poleni kwa misiba iliyowaandama. Kuwapoteza wapendwa si pigo kwa familia tu, bali pia kwa kijiji na taifa. Na kuanzia sasa ninawaomba tushirikiane kuibadilisha hali hii. Hatuwezi kuendelea kuishi hivi," alisema huku wanakijiji wanamtazama kwa masikitiko makubwa.

"Binadamu yumo katika awamu ya kujiangamiza", aliendelea, "amefanya uvumbuzi wa teknolojia aali lakini ambayo sawa na mwaridi, ina miba. Miba hii sasa inamchoma kila aitundaye teknolojia. Kwa sababu ya wingi wetu, sasa tunataka kuzalisha mazao yetu haraka. Kwa sababu ya ongezeko kubwa la idadi ya watu walaji ni wengi lakini ardhi inazidi kujibana. Njia ya pekee ya kuongeza lishe ni kupitia uzalishaji zaidi wa vyakula. Katika ulimwengu ambapo vipando vile vile hurudiwa kupandwa kwenye ardhi ile ile, pato lake hupungua. Jibu la kuinua pato ni teknolojia. Teknolojia hii imebuni uzalishaji wa mbolea ya kemikali ambazo huchochea rotuba kwenye ardhi. Urutubishaji wa ardhi yetu ndogo umetuwezesha kuzalisha chai, kahawa, mahindi na mazao mengine kwa wingi ili kukidhi haja yetu ya chakula. Zamani ardhi ilipokuwa kubwa na idadi ya watu ikawa ndogo, haja hii ya mbolea haikuwepo. Ardhi iliachwa kujirutubisha yenyewe. Madhara tuyaonayo sasa hayakuwepo wakati huo."

"Leo hii utashi wetu wa kujitosheleza umetusukumizia ukingoni mwa maisha. Vyakula vyetu sasa vina kemikali hatari kutokana na mizizi ya mimea kufyonza virutubisho vyenye nitrojeni. Virutubisho hivi hustawisha mimea. Hata hivyo mimea hii tunayoila ina kemikali hatari kwa miili yetu. Kemikali hizi vilevile huingia kwenye nyasi ambazo huliwa na mifugo wetu. Mifugo hao hudhurika, nasi tunapofaidi bidhaa zao tunadhurika. Hata mito yetu na visima hupokea mikusanyiko ya kemikali hizi hatari, nasi tunazinywa kupitia kwa maji. Kemikali hizi husababisha saratani, na hili ndilo tatizo la kijiji hiki."

Kauli hii ya mwisho iliutikisa umati ule. Sauti za wanakijiji zilisikika zikinong'onezana. Wengi wa wanakijiji waliona kama kila kitu pale kijijini kilikuwa chanzo cha adhabu ya kifo kwao.

Baada ya kule kutanabahishwa, ilisikika sauti ya mlevi mmoja aliyesema kwa sauti kubwa kabisa, "Ni hivi, ama tule hivyo vibaya tufe polepole au tuache kuvila tufe mara moja."

Tamko hili la mlevi liliwasisimua wote waliokuwa pale, wakapata walau sababu ya kucheka. Kucheka huku kuliwatia watu matumaini, wakaanza kuuliza maswali. Kwa nini mbolea itengenezwe kutokana na kemikali hatari? Hivi dunia haijui kuwa ipo hatari kwenye mbolea hizo? Je, waache kunywa maji na kutupa vyakula walivyokuwa navyo? Waliuliza maswali haya na mengine mengi.

Downloaded from https://kcse.org

Yule mtaalamu hakuwa na mengi ya kusema kwa sababu alifahamu kuwa kila aina ya teknolojia ina faida na madhara yake. Kwa hivyo alieleza kwa ufupi.

"Kemikali hizo ndizo huchochea rutuba ya ardhi ambayo huiwezesha mimea kukua na kutupa mazao mengi. Dunia inafahamu fika madhara ya kemikali zinazotumiwa kwenye mbolea lakini ifanyeje? Watu watakao kulishwa ni wengi. Ardhi imepungua kwa sababu ya wingi wa watu. Watu wanataka kula ilhali ardhi hiyo ndogo haina tena rutuba. Hata maji hayo yaliyoathirika mtayanywa tu bado. Mtaishije bila maji? Mtapika vipi? Mtakunywa nini? Hali hii tunaweza kuiondoa polepole kwa kuwekeza kwenye ufugaji wa kuku, ng'ombe na mbuzi wengi ili tutumie mbolea yao kurutubisha ardhi yetu. Wanasayansi wanasema itachukua yapata miaka mitano kuirejesha ardhi katika hali yake asilia."

Maelezo ya mtaalamu yule yalileta nafuu ya namna fulani kwa wanakijiji. Mzee mmoja alipewa nafasi kuzungumuza kabla ya kikao kufungwa. Mkutano ulipomalizika kijiji kilijua tatizo lilipokuwa na kuumaliza uvumi uliokuwa unaoteshwa kila leo.

(a) Eleza sababu **mbili** za wanakijiji kuuona ugonjwa uliozuka kuwa miujiza. (alama 2)

(b) Eleza madhara **manne** ya kemikali za mbolea kulingana na kifungu. (alama 4)

(c) Bainisha mambo **matatu** yanayochochea kubuniwa kwa teknolojia mpya kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

(d) Andika mambo **mawili** yanayoonyesha kuwa wazee wa jamii hii walikuwa na hadhi. (alama 2)

(e) Fafanua maana ya 'nywele za koto' na 'nywele za singa' kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 2)

(f) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 2)

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Demokrasia ni mfumo wa utawala ambapo wananchi huwa na mamlaka ya kuwachagua wawakilishi wao moja kwa moja. Demokrasia ni utawala wa umma. Utawala huu ni tofauti na utwala wa mtu mmoja au wa kundi dogo. Katika serikali ya kidemokrasia, umma huhakikishiwa haki fulani za kimsingi ambazo haziwezi kukiukwa au kutupiliwa mbali. Kwa kawaida haki hizo hutambuliwa na kudhibitiwa kimataifa.

Kwa mujibu wa Larry Diamond, demokrasia ina mihimili kadhaa. Demokrasia inashirikisha kuchagua na kubadili serikali kupitia chaguzi za huru na haki. Inahusu pia kuhusika kikamilifu kwa umma katika siasa na masuala ya kijamii kwa jumla. Kadhalika, demokrasia inahusu kulindwa kwa haki za kibinadamu za wananchi. Ni utawala ambao huongozwa na sheria, na ambapo sheria na taratibu zake hutumiwa kwa namna sawa kwa wananchi wote. Ni muhimu kutaja kwamba, kila nchi huifasiri dhana ya demokrasia kwa namna inavyoifaa yenyewe. Kwa mfano, katika taifa la Kenya, demokrasia ni serikali ya wananchi ikiongozwa na wananchi kwa niaba ya wananchi.

Zipo aina mbalimbali za demokrasia. Demokrasia ya moja kwa moja huhusu wananchi kupigia sera fulani kura moja kwa moja bila kupitia kwa wajumbe au wawakilishi. Aina hii ya demokrasia huwezekana pale ambapo nchi ina idadi ndogo ya watu, hasa ambao wamesoma na wana mambo mengi yanayoshabihiana. Aina hii ya demokrasia ndiyo inayotumiwa Uswisi.

Downloaded from: https://atikaschool.co.ke

Kuna mataifa ambapo wananchi huwachagua wawakilishi wao wa bunge. Hii huitwa demokrasia ya uwakilishi au isiyo ya moja kwa moja. Hii ndiyo aina ya demokrasia inayotumika sana na hutilia mkazo ulinzi wa haki za wote; wawe wachache au wengi. Hutilia maanani matakwa ya watu binafsi kuliko yale ya taifa zima. Mfano mzuri wa demokrasia hii ni India. Demokrasia ya uwakilishi huweza kujitokeza kwa namna tofautitofauti kutegemea matakwa ya nchi mahususi.

Demokrasia ya Urais ni aina mojawapo ya demokrasia ya uwakilishi. Aina hii ya demokrasia humpa rais mamlaka makuu juu ya serikali. Rais huchaguliwa ama kwa njia ya moja kwa moja, au kwa kutumia wawakilishi. Yeye hawi tu kiongozi wa taifa, bali pia wa serikali kama ilivyo Kenya, Marekani na Ajentina. Hali kadhalika, kuna Demokrasia ya Bunge. Aina hii huipa bunge mamlaka makubwa. Kitengo cha utekelezi cha serikali hupata mamlaka yake kutoka bungeni. Kiongozi wa taifa na kiongozi wa serikali huwa watu tofauti na wenye viwango tofauti vya mamlaka. Kwa kawaida, kiongozi wa serikali huwa na mamlaka makubwa zaidi kama ilivyo Uingereza. Demokrasia ya kimabavu huelekea kupingana na dhana halisi ya demokrasia. Katika demokrasia hii tabaka la juu pekee ndilo lenye haki ya kuchagua wawakilishi wa taifa. Umma hauna haki hiyo. Mfano wa demokrasia hii ni Urusi.

Demokrasia ina manufaa mengi. Demokrasia hulinda masilahi ya wananchi wote; si walio wengi, si walio wachache, si wenye nguvu, si wanyonge. Demokrasia pia husaidia kugatua mamlaka, hivyo kuzuia kundi dogo kuwa mamlakani daima. Hili hufanikishwa na chaguzi za mara kwa mara. Kwa vile sheria haibagui, demokrasia basi hukuza usawa kwa wote. Wale wanaochaguliwa hujaribu kuweka sera mwafaka kwa kuwa hawadumu mamlakani. Kuhusishwa kwa umma katika kuamua watakaowatawala na kuwepo kwa kipindi mahususi cha kuhudumu hupunguza uwezekano wa kutokea kwa mapinduzi.

Hali kadhalika, demokrasia huchochea mabadiliko katika nchi kwa kuwa kila utawala huwa na kipindi chake maalumu ambapo umma hupata nafasi ya kuubadilisha, na hivyo kubadili sera na mwelekeo wa nchi. Demokrasia huipa umma nafasi ya kujifunza mambo mengi kuhusu siasa. Wakati wa uchaguzi, wagombeaji hunadi sera na rawaza zao, na hivyo kuelimisha umma. Demokrasia pia huwafanya watawala kuwa na tahadhari na kuwajibika kwa kuwa umma ulioerevuka kisiasa unawatia kwenye mizani na huenda usiwachague tena.

Ni dhahiri kwamba demokrasia ina dhima kuu katika maendeleo ya nchi. Hivyo ipo haja ya kuthamini na kuendeleza mifumo ifaayo ya kidemokrasia ili kuhakikisha kwamba haki ya kila raia imelindwa.

(a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 110. (alama 10)

(b) Kwa maneno 50, eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 5)

Downloaded From: https://atikaschool.org

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

(i) irabu, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu

(ii) konsonanti, konsonanti, irabu, irabu

(b) Ainisha mofimu katika maneno yafuaatayo: (alama 2)

(i) asemavyo

(ii) mwangwi

(c) Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Shule nzima ilifurahia ukarimu wa Shirika la Tugawane.

(d) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)

Seremala aliulainisha ubao huo ili kutengeneza kasha amuuzie mlinzi huyo.

(e) Tunga sentensi ukitumia vivumishi vinavyotoa maana zifuatazo:

(i) Nafasi katika orodha (alama 1)

(ii) Kutobagua (alama 1)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa. (alama 1)

Mtu huyo alifuata njia iliyomwelekeza mjini.

(g) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo bila kupoteza maana.

(i) Mhandisi alikarabati mtambo.
Mtambo ulikuwa kiwandani.
(Unganisha kuwa sentensi moja bila kutumia kiunganishi.) (alama1)

(ii) Kembo alishona fulana hiyo <u>vizuri</u> <u>sana</u>. (Tumia kielezi cha kiasi badala ya vile vilivyopigiwa mstari.) (alama 1)

(h) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 2)

Mkurugenzi alisema kwamba wangetoa nyongeza ya mshahara mwaka ambao ungefuata.

(i) Geuza sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 1)

Ni wazi kwamba gharama ya maisha itapanda bei ya mafuta ikipanda.

Downloaded From: https://atkaschool.org

(j) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi. (alama 1)

Badi huwa hapitii hapa, huenda usimpate.

(k) Zuri ni kwa baya, aminifu ni kwa ..... na vivu ni kwa ..... (alama 2)

(l) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) sukari .....

(ii) teo .....

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari. (alama 2)

Mvua imepusa na watu wameanza kuondoka.

(n) Vyakula viliandaliwa. Vyakula vilikuwa na viinilishe muhimu.
(Unganisha kuunda sentensi changamano.) (alama 2)

(o) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama3)

Zumari alimtunzia Keto watoto hao kwa upendo.

(p) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** ya kiambishi '**ku**'. (alama 2)

(q) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Usalama ukiimarishwa watalii wengi watakuwa wanazuru humu.

(r) Unaporidhika na jambo unasema hewala, unaposhangilia timu yako kwa kupata ushindi unasema ..... na unapotaka usikivu unasema ..... (alama 2)

(s) Jepesi ni kwa rahisi, ukuta ni kwa ..... na njia ni kwa ..... (alama 2)

(t) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **dua** na **tua**. (alama 2)

(u) Mzee Pumu ni mraibu wa vileo. Baada ya muda watoto wake wawili wanakuwa watumizi sugu wa vileo. Andika methali inayoweza kutumiwa kuelezea hali hii. (alama 1)

(v) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha uteuzi. (alama 1)

4. ISIMUJAMII (Alama 10)

Wewe ni mhubiri katika Maabadi ya Shamu. Umealikwa kuwahubiria wanafunzi wa Shule ya Upili ya Lulu. Fafanua sifa **kumi** za lugha utakayotumia.

Downloaded From: https://atikaschool.org

4.2.3 Kiswahili Paper 3

SEHEMU A: RIWAYA

A. Matei: *Chozi la Heri*

1. Lazima

(a) "Sasa haya ameyapa kisogo ... kufunguliwa kwa kituo hiki ni kama mana iliyomdondokea kinywani kutoka mbinguni."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha tamathali **mbili** za usemi ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Fafanua umuhimu wa mhusika anayerejelewa katika dondoo hili katika kuijenga riwaya hii. (alama 6)

(b) Jadili mikakati mwafaka ambayo vijana wanatumia kukabiliana na hali yao ya maisha kwa kuwarejelea wahusika wafuatao:

(i) Chandachema (alama 4)

(ii) Dick (alama 4)

SEHEMU B: TAMTHILIA

P. Kea: *Kigogo*

Jibu swali la 2 au la 3

2. (a) Jadili mbinu **kumi** ambazo Wanasagamoyo wanatumia kupigana na utawala dhalimu. (alama 10)

(b) Eleza jinsi mbinu rejeshi ilivyotumiwa kukuza vipengele vifuatavyo katika tamthilia hii.

(i) Maudhui (alama 5)

(ii) Wahusika (alama 5)

3. (a) "Ushahidi utatoka wapi kama kipanga ndiye hakimu kwenye kesi ya kuku?"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Fafanua dhima ya vipengele **viwili** vya kimtindo vinavyobainika katika dondoo hili. (alama 4)

(b) (i) Kwa kurejelea tamthilia jadili sifa **sita** za msemaji. (alama 6)

(ii) Eleza umuhimu wa mandhari katika tamthilia hii. (alama 6)

Downloaded From: https://atikasdool.org

SEHEMU C: HADITHI FUPI

Jibu swali la 4 au la 5

A. Chokocho na D. Kayanda (Wah): *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

K. Walibora: "Nizikeni Papa Hapa"

4. (a) "Isije ikawa hapa habari ya kufuata asali ukafa mzingani." "... Pana hasara gani nzi kufia kidondani?"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)

(ii) Andika mbinu **mbili** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(b) Hadithi, *Nizikeni Papa Hapa* inahimiza uwajibikaji. Jadili. (alama 6)

(c) Eleza jinsi maudhui ya umaskini yanavyojitokeza katika hadithi, *Mapenzi ya Kifaurongo.*" (alama 7)

A.Chokocho: "Shogake Dada ana Ndevu"

5. (a) Onyesha jinsi unafiki unavyoshughulikiwa katika hadithi, "*Shogake Dada ana Ndevu.*" (alama 8)

(b) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 12)

"Bi. Hamida alitunga donge kifuani mwake. Na donge likaja juu. Likampanda na kumsakama kooni. Kweli? Uongo? Kweli au uongo yale maneno ya binti yake? Labda kweli anamfikiria mambo mabaya binti yake tu. Labda kweli dhana yake ni mbovu. Bi. Hamida alichanganyikiwa na mambo. Alivutwa huku na huku na nafsi yake yenye chagizo. Upande mmoja sauti yake ya ndani ilikuwa inamtetea Safia, na upande wa pili wa nafsi yake ilikuwa ikimshuku Safia; na sauti zake zote mbili hizo zimo ndani ya kiwiliwili chake zinamvuta yeye mtu mmoja, Bi. Hamida. Hatimaye hakutambua afanye nini."

Downloaded From: https://atkaschool.org

SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7.

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Lilipo lile banda, lile pale,
Kuna mja kakonda, kwa uwele,
Wala siye kupenda, hiyo ndwele,
Ndwele ya kutwishwa!

Ni ndwele ya kutengwa, penye haki,
Uwele wa kusutwa, pasi haki,
Ugonjwa kupuuzwa, na miliki,
Ndwele ya kutwishwa!

Mwiliwe kawa sugu, viwandani,
Uso una kunyugu, ziso fani,
Ujira wake ndugu, ni mapeni,
Ndwele ya kutwishwa!

Na homa akipatwa, maishani,
Kwa tiba apuuzwa, kama nyani,
Hajulikani kuwa, yeye nani,
Ndwele ya kutwishwa!

Ana chawa nyweleni, ona dhiki,
Na kunguni nguoni, ahiliki,
Funza na miguuni, wamesaki,
Ndwele ya kutwishwa!

Bado yuasubiri, kisimati,
Dhiki yake kutiri, 'we tamati
Ndipo iwe sururi, ya kidhati
Nyota yake ni nyota ya huzuni.

(K.Wamitila)

(a) Fafanua kwa kutoa hoja **sita** kutoka kwenye shairi, jinsi nyota ya anayerejelewa ni ya huzuni. (alama 6)

(b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

(c) Bainisha aina zifuatazo za uhuru wa kishairi katika shairi: (alama 2)

(i) inkisari

(ii) kufinyanga sarufi

Downloaded From: https://atikaschool.org

(d) Eleza tamathali **tatu** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

(f) Eleza sifa **mbili** za anayelengwa katika shairi hili kwa kurejelea ubeti wa mwisho. (alama 2)

(g) Andika ubeti wa **nne** kwa lugha nathari. (alama 2)

7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Kama akili si mali, maskini na tajiri
Wangalimoja sampuli, asikuwepo fakiri
Na hangekuwa na mali, mwinyi bila kufikiri
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Ukeshapo kwa fikara, ni kwa wingi wa akili
Kuwaza kigaragara, una mengi si kalili
Na kuwa una tambara, metajirika kwa hili
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Alokijenga kitanda, ana wingi wa akili
Hata asiwe na bunda, hamithili kwa akili
Hata naye paka nunda, pasipo akili hali
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Akili kweli ni mali, kwa kuteua vya mwozo
Singetumia akili, ungevila vya angamizo
Afya ikawa thakili, na kuhiliki mawazo
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Vipi gonjwa kikuganda, wawazia spitali?
Huachi ukawa ng'onda, ukanyauka muwili
Ugangani unakwenda, kutafuta afadhali,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Kama akili si mali, kusingekuwa na jela,
Kuwatenga kuwa mbali, wenye hiana na hila,
Kwa mbavu na ufidhuli, pamwe mbinu tolatola,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Tajiri na maskini wote wanayo akili,
Ni kuwa hayafanani, waliyonayo makali
Kabisa hawashibani, liwe lile au hili,
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

Downloaded From: https://atikaschool.org

Kama akili si mali, 'singekuwa na hazina
Ya kudadisi mithali, na kupinga yako mana
Gani inadumu mali, kuliko huko kusana?
Kama akili si mali, usingeweza fikiri.

(T. Arege)

(a) "Ufanisi wa binadamu hutegemea akili." Fafanua kwa kurejelea hoja **sita** kutoka kwenye shairi hili. (alama 6)

(b) Andika mifano ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili: (alama 4)

(i) sitiari

(ii) tanakuzi

(iii) swali la balagha

(iv) kinaya

(c) Eleza mbinu **nne** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

(d) Andika aina **mbili** za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 2)

(e) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Shangazi anambila
umewadia muda
wa kukiacha kiambo
cha Baba
Nende kujinasibisha
na ajinabi tusohusiana
kwa ngeu wala usaha
nache niwapendao
nache aila
nache matamanio
ya elimu kufuatiya.

Anambile shangazi
Hino ni neema
ela moyo wanirai
"Wajitia shemere", nami nauambia,
"Najua si utashi wangu"
ila hiari sina

Downloaded From: https://jaikaschool.org

kwani hii ni faradhi
mitamba mepokelewa
na ami kwa furaha
kilobaki ni kuvuka
kizingiti hiki."
Kwaheri Mama, kwaheri wanuna.

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 2)

(b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. (alama 2)

(c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. (alama 6)

(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.

(i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. (alama 5)

(ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. (alama 5)

Downloaded From: https://atikaschool.org